TANGAZO LA SERIKALI Na....... la tarehe 10/12/2010

# SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

## SURA 288

## SHERIA NDOGO

Zimetungwa Chini ya Kifungu cha 89

## SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII – TIBA KWA KADI) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO, 2010

Jina na mwanzo wa kutumika

1 Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Uanzishaji Mfuko wa Afya ya Jamii – Tiba kwa Kadi) (TIKA) za Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, 2010 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye gazeti la serikali.

Matumizi

2 Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

Tafsiri

3 Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo,

"Ada ya mtumiaji" maana yake ni ada inayotozwa na Hospitali, Kituo cha Afya au Zahanati, kwa ajili ya Huduma ya Afya iliyotolewa kwa mtumiaji.

"Asasi" ni pamoja na shule, vyuo, vikundi mbalimbali vilivyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria au Asasi yoyote itakayokuwa imekubaliwa na kuidhinishwa na Bodi.

Sura ya 288

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri iliyoundwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

"Huduma za Afya" maana yake ni huduma zote za afya zinazotolewa na Hospitali wa Serikali na watu binafsi na zinajumuisha huduma nyingine za afya zilizoanzishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma za afya ikiwa ni pamoja na Vituo vya Afya na Zahanati.

"Kadi" maana yake ni kadi itakayotolewa na Bodi kwa mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

"Kaya" maana yake ni:

(a) mama, Baba na watoto wenye umri chini ya miaka kumi na minane;

(b) mwanachama yeyote aliyefikia umri wa miaka kumi na minane au zaidi na awe na mtoto au bila mtoto mwenye umri chini ya

miaka kumi na minane

(c) Taasisi yoyote.

"Kituo cha huduma kilichoteuliwa" maana yake ni kituo kinachotoa Huduma za Afya na ni pamoja na kituo chochote kilichoanzishwa au kinachoendesha kwa malengo ya kutoa huduma za afya kiwe kinamilikiwa na Halmashauri, Serikali, Asasi za Kidini, mtu au watu binafsi ambacho kinahusika na Mfuko wa Afya ya Jamii.

"Mchango au ada ya mwanachamna" maana yake ni mchango wa hiari utakaotolewa na wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

"Mganga Mkuu" maana yake ni Daktari ambaye ni Msimamizi Mkuu wa shughuli zote za huduma za afya katika Manispaa.

"Mwanachama" maana yake ni kaya inayochangia kwenye Mfuko wa Afya ya Jamii.

"Malipo ya huduma" maana yake ni malipo yanayotozwa na kituo cha tiba, kilichoteuliwa kwa watu ambao sio wanachama, wanapopatiwa huduma za afya katika kituo hicho.

"Mfuko au Mfuko wa Afya ya Jamii" maana yake ni mfuko wa afya ya jamii wa tiba kwa kadi (TIKA) ulioanzishwa chini ya sheria hii.

"Tele kwa Tele" maana yake ni mkataba unaoeleza wajibu wa Halmashauri na wajibu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika utekelezaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

"Wizara" maana yake ni Wizara yenye dhamana ya masuala ya afya.

Mfuko wa Afya ya Jamii

4 (1) Kutakuwa na Mfuko wa Afya ya Jamii wa Tiba kwa Kadi (TIKA) ambao ni mfuko wa hiari wenye lengo la kutoa huduma za afya, ambapo kaya zitakuwa zikilipia huduma hizo na Serikali itatoa mchango wake wa fedha kama jazilio kwa mchango kutoka kwenye kaya (Tele kwa Tele).

(2) Matumizi ya fedha yatafanywa na kusimamiwa na Bodi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Madhumuni ya Mfuko

5 Madhumuni ya Mfuko yatakuwa ni:

(a) kutafuta vyanzo vya fedha kutoka katika jamii kwa ajili ya kutoa huduma bora za afya kwa wanachama.
(b) kutoa huduma bora za afya zinazopatikana kwa kutumia mipango endelevu; na
(c) kuboresha huduma za afya katika jamii kwa kugawanya madaraka na kuzipa nguvu jamii katika kufanya maamuzi na kuchangia katika masuala yanayohusu afya zao.

Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii

6 (1) Kutakuwa na Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi baada ya kupokea mapendekezo kutoka Timu ya Uendeshaji ya Halmashauri.

(2) Majukumu ya Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii yatakuwa kama ifuatavyo:

(a) kufuatilia, kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii kwenye vituo vya kutolea Huduma za Afya ya Jamii.
(b) kuwa kiungo kati ya Halmashauri, Jamii na Wadau mbalimbali kwa ushirikiano na Mhasibu wa Mfuko, na
(c) kuandaa taarifa za Mfuko wa Afya ya Jamii za robo, nusu mwaka pamoja na majukumu mengine atakayopangiwa na Halmashauri.

Muundo wa Bodi

7 Bodi itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) wawakilishi wanne wa watumiaji huduma za afya kati yao wawili ni lazima wawe ni wanawake;
(b) mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za Afya binafsi bila faida
(c) ~~mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za afya binafsi kwa faida~~ waliochaguliwa na Halmashauri kutoka vituo vya kutolea huduma za afya binafsi kwa faida waliochaguliwa miongoni mwao; na
(d) mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya.

Wataalam ambao hawatapiga kura:
(a) Afisa Mipango wa Manispaa;
(b) Mganga Mkuu wa Manispaa ambaye atakuwa Katibu wa Bodi.
(c) Mwakilishi mmoja kutoka Hospitali inayotoa huduma ndani ya Manispaa
(d) Mwakilishi mmoja kutoka Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa.

Mwenyekiti wa Bodi atachaguliwa miongoni mwa Wajumbe waliotajwa katika (1) (a) – (c).

Kazi zaBodi

8 Ili kufanikisha malengo yake makuu, Bodi itakuwa na kazi zifuatazo:
(a) kusimamia masuala na shughuli zote zinazohusu Mfuko wa Afya ya Jamii.
(b) Itafanya kazi kwa kushauriana na Timu ya Uendeshaji ya Huduma za Afya ya Halmashauri na kuhakikisha kuwa huduma ya afya inayotolewa ni bora na ya kitaalamu;
(c) kukusanya na kusimamia mapato ya Mfuko wa Afya ya Jamii.
(d) kupendekeza kwa Halmashauri watu wanaostahili kusamehewa kutoa mchango kwenye mfuko.
(e) kuweka malengo ya Mfuko.

Sifa za Wajumbe wa Bodi

9 Mjumbe wa Bodi atakuwa na sifa zifuatazo:
(a) awe raia wa Tanzania isipokuwa kwa Wawakilishi kutoka

**Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii**

6 (1) Kutakuwa na Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi baada ya kupokea mapendekezo kutoka Timu ya Uendeshaji ya Halmashauri.

(2) Majukumu ya Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii yatakuwa kama ifuatavyo:

(a) kufuatilia, kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii kwenye vituo vya kutolea Huduma za Afya ya Jamii.
(b) kuwa kiungo kati ya Halmashauri, Jamii na Wadau mbalimbali kwa ushirikiano na Mhasibu wa Mfuko, na
(c) kuandaa taarifa za Mfuko wa Afya ya Jamii za robo, nusu mwaka pamoja na majukumu mengine atakayopangiwa na Halmashauri.

**Muundo wa Bodi**

7 Bodi itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) wawakilishi wanne wa watumiaji huduma za afya kati yao wawili ni lazima wawe ni wanawake;
(b) mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za Afya binafsi bila faida
(c) mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za afya binafsi kwa faida waliochaguliwa na Halmashauri kutoka vituo vya kutolea huduma za afya binafsi kwa faida waliochaguliwa miongoni mwao; na
(d) mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya.

Wataalam ambao hawatapiga kura:
(a) Afisa Mipango wa Manispaa;
(b) Mganga Mkuu wa Manispaa ambaye atakuwa Katibu wa Bodi.
(c) Mwakilishi mmoja kutoka Hospitali inayotoa huduma ndani ya Manispaa
(d) Mwakilishi mmoja kutoka Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa.

Mwenyekiti wa Bodi atachaguliwa miongoni mwa Wajumbe waliotajwa katika (1) (a) – (c).

**Kazi zaBodi**

8 Ili kufanikisha malengo yake makuu, Bodi itakuwa na kazi zifuatazo:
(a) kusimamia masuala na shughuli zote zinazohusu Mfuko wa Afya ya Jamii.
(b) Itafanya kazi kwa kushauriana na Timu ya Uendeshaji ya Huduma za Afya ya Halmashauri na kuhakikisha kuwa huduma ya afya inayotolewa ni bora na ya kitaalamu;
(c) kukusanya na kusimamia mapato ya Mfuko wa Afya ya Jamii.
(d) kupendekeza kwa Halmashauri watu wanaostahili kusamehewa kutoa mchango kwenye mfuko.
(e) kuweka malengo ya Mfuko.

**Sifa za Wajumbe wa Bodi**

9 Mjumbe wa Bodi atakuwa na sifa zifuatazo:
(a) awe raia wa Tanzania isipokuwa kwa Wawakilishi kutoka

Mashirika ya Dini na Taasisi zisizo za Kiserikali.

(b) awe na umri si chini ya miaka ishirini na tano na si zaidi ya miaka sabini awe na akili timamu.

(c) awe amehitimu elimu ya sekondari na kuendelea;

(d) awe na uzoefu na amewahi kuonyesha uwezo wake wa kuongoza katika shughuli za huduma ya jamii.

(e) awe na sifa za uongozi; na

(f) asiwe na wadhifa wowote wa kisiasa wa chama chochote cha siasa.

*Muda wa kukaa madarakani*

10 (1) Mjumbe wa Bodi atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe aliyochaguliwa na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha miaka mitatu tu.

(2) Endapo nafasi yoyote ya mjumbe wa Bodi itaachwa wazi kwa sababu ya kifo, kujiuzulu kukiuka maadili ya kazi au ulemavu utakaomfanya ashindwe kushiriki kikamilifu kama mjumbe au kwa sababu nyingine yoyote ile, mjumbe mwingine atachaguliwa kujaza nafasi hiyo iliyoachwa wazi.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2), haitaruhusiwa kuchagua mjumbe mwingine iwapo kipindi kilichobaki ni chini ya miezi sita.

*Mkutano wa Bodi*

11 (1) Mikutano ya kawaida ya Bodi itaitishwa na Mwenyekiti kila robo mwaka.

(2) Ikiwa kuna umuhimu, Mwenyekiti anaweza akaitisha kikao cha dharura kulingana na mahitaji maalum.

*Uwajibikaji wa Bodi*

12 Bodi itawajibika kwa Halmashauri kupitia Kamati husika.

*Vyanzo vya mapato*

13 Vyanzo vya mapato ya Mfuko vitatokana na:

(a) fedha zote zitakazopokelewa kutokana na michango ya wanachama;

(b) ruzuku kutoka kwenye Halmashauri, Serikali Kuu na wahisani mbalimbali kutoka ndani na nje ya Halmashauri.

(c) michango ya watu binafsi wanaoishi ndani na nje ya Halmashauri.

(d) malipo ya fedha ya wasiokuwa wanachama wa Mfuko kwa kupata huduma ya afya;

(e) ushuru utakaotozwa na Halmashauri kutoka vyanzo mbalimbali na kutengwa kwa ajili ya Mfuko; na

(f) fedha zozote halali ambazo Mfuko unaweza kupata toka mahali pengine popote.

*Akaunti ya Mfuko au Bodi na watiaji saini*

14 (1) Kutakuwepo na akaunti maalum ya Halmashauri itakayotumika na Bodi ambayo fedha zote zitakazokusanywa kwa ajili ya Mfuko zitahifadhiwa na kutolewa.

(2) Malipo yataidhinishwa na Mkurugenzi kwa kufuata taratibu na kanuni za fedha za Halmashauri.

(3) Watiaji saini wa akaunti ya Mfuko watachaguliwa na Bodi na watakuwa ni mmoja kutoka kundi "A" na "B" na kwa namna yoyote hakuna fedha zitakazotolewa kwenye akaunti ya mfuko bila saini ya mmojawapo kutoka kundi "A" na "B"

(4) Watia saini kwenye hundi za Mfuko watakuwa kama ifuatavyo:
   (a) mwenyekiti wa Bodi na mjumbe mmoja wa Bodi ambao watakuwa Kundi "A"
   (b) katibu wa Bodi ambaye atakuwa ni Mganga Mkuu wa Manispaa na Mweka Hazina wa Manispaa ambao watakuwa Kundi "B".

(5) Kila baada ya miezi mitatu, Bodi itakuwa inatoa taarifa ya akaunti ya Mfuko kama itakavyokuwa imeagizwa na Halmashauri.

(6) Akaunti ya Mfuko itakaguliwa na Wakaguzi waliochaguliwa kwa mujibu wa Kanuni za fedha za Serikali za Mitaa.

(7) Kila kituo cha Huduma za Afya kinaweza kufungua akaunti kwa ajili ya matumizi ya fedha ya shughuli za afya. Akaunti hizo zitasimamiwa na Kamati za usimamizi wa Vituo husika. Aidha, vitafuata taratibu na kanuni za fedha za Halmashauri.

Taarifa ya mwaka ya fedha

15 Mwezi mmoja baada ya mwaka wa fedha wa Halmashauri, Bodi itatakiwa kuandaa taarifa ya mapato na matumizi ya fedha na kuiwasilisha kwa Halmashauri mapema iwezekanavyo.

Mipa... na matu...

16 (1) Miezi miwili kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha wa Halmashauri, Bodi itaandaa mipango na bajeti ya mwaka kwa kuonyesha kiwango kinachotarajiwa kupatikana na mgawanyo wa fedha kwa ajili ya utoaji huduma za afya na maendeleo katika maeneo ya Halmashauri.

(2) Bodi inaweza kuandaa bajeti ya nyongeza kama kutakuwa na haja ya kufanya hivyo na kama mazingira yataruhusu;

(3) Mipango ya bajeti ya Mfuko itaandaliwa kulingana na utaratibu kama ilivyoainishwa katika vifungu vidogo vya (1) na (2) hapo juu, ambayo ni lazima iwasilishwe kwa Halmashauri kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi.

(4) Matumizi yatazingatia mipango shirikishi ya maeneo husika ambayo itakuwa sehemu ya Mpango Kabambe wa Afya wa Halmashauri. Pia mipango hii itazingatia maelezo yaliyomo ndani ya Mkataba wa Tele kwa Tele.

(2) Kamati ya Afya ya Kata, itakaa kila baada ya miezi mitatu na Katibu atatoa taarifa ya maandishi kwa wajumbe wiki moja kabla ya siku ya kikao.

**Matumizi ya fedha za Mfuko**

21 Fedha zitakazokusanywa na Mfuko zitatumika kwa madhumuni yafuatayo:

(1) Masuala yanayohusiana na afya yaliyotajwa katika Mpango wa Afya wa Halmashauri na kuidhinishwa na Wizara; na

(2) Suala au shughuli yoyote muhimu ya afya kama itakavyoonekana inafaa na kama itaidhinishwa na Bodi.

**Utoaji wa Kadi kwa wanachama**

22 (1) Kila mwanachama wa Mfuko na wategemezi wake, atapewa Kadi baada ya kulipa mchango wake wa mwaka kama ulivyoainishwa katika kifungu cha 23 (1) cha Sheria Ndogo hizi.

(2) Kwa kuzingatia kanuni za Mfuko wa Afya ya Jamii za mwaka 2004, kila mtu atakayepewa msamaha ni lazima atapewa kadi ya uanachama, na Halmashauri husika itaweka utaratibu wa kulipia kadi hiyo.

**Haki za mwanachama na utoaji wa huduma za afya**

23 (1) Kila mwanachama na wategemezi wake watakuwa na haki ya kisheria kupata huduma ya afya aliyolipia kabla ya kuugua ndani ya eneo la Halmashauri au katika kituo cha Halmashauri nyingine ambayo itaingia makubaliano maalum na Halmashauri.

(2) Huduma ya afya kwa Baba, Mama na Watoto wao wenye umri chini ya miaka kumi na minane.

(3) Kutoa mapendekezo kuhusu huduma za afya kupitia kituo chake cha tiba ambayo yatafanyiwa kazi na Bodi; na

(4) Kushirikishwa kikamilifu katika uandaaji na utekelezaji wa mpango wa upatikanaji wa huduma za afya, katika eneo la Halmashauri.

**Kiwango cha mchango au ada ya mwanachama**

24 (1) Mwanachama wa mfuko wa afya ya jamii atapaswa kulipa kila mwaka mchango kiasi cha shilingi elfu kumi tu (10,000/=);

(2) Mchango huo utalipwa na kila mtu anayetaka kuwa mwanachama wa mfuko mwanzoni mwa mwaka au kila mwaka wa fedha unapoanza au kama Bodi itakavyoelekeza;

(3) Mwanachama ana hiari ya kulipa mchango wake wa uanachama kwa zaidi ya mwaka mmoja;

(4) Halmashauri itaandaa utaratibu wa kupanga kaya maalum katika Asasi mbalimbali kwa mfano: Shule zilizoko katika Halmashauri.

(5) Bila kuathiri kifungu kidigi cha (3) hapo juu, mwanachama anayelipa mchango wa uanachama kwa zaidi ya mwaka mmoja, pale inapotokea mabadiliko ya kiwango cha mchango atawajibika kulipa tofauti ya kiwango alicholipa na kila cha awali.

Muda wa uanachama

25 (1) Mwanachama atabaki kuwa mwanachama wa Mfuko wa Afya ya jamii na tiba kwa kadi kila atakapolipa ada yake ya mwaka ya uanachama.

(2) Uanachama utafikia mwisho pale mwanachama asipotimiza masharti ya kifungu (1) hapo juu.

Malipo ya papo kwa papo

26 (1) Mtu yeyote ambaye hatakuwa mwanachama wa mfuko huu, atalipa mchango au malipo ya papo kwa papo kila atakapoenda kupata matibabu katika kituo cha kutolea huduma za afya.

(2) Malipo ya hapo kwa papo yatalipwa kama ifuatavyo:

(a) Shilingi elfu moja (1,000/=) katika huduma za Afya zinazotolewa na Zahanati katika eneo lolote la Halmashauri;
(b) Shilingi elfu mbili (2,000/=) kwa huduma za Afya zinazotolewa na Kituo cha Afya kilichopo ndani ya Halmashauri.
(c) Huduma za hospitali za aina zote kulingana na Sera ya uchangiaji.

Kamati ya Afya ya Zahanati na kamati zingine

27 Kamati ya afya ya zahanati na Kamati zote zilizoundwa chini ya Hati Rasmi ya Uanzishaji wa Bodi, zitafanya kazi katika Mfuko huu kwa kuzingatia Sheria Ndogo hizi.

Utaratibu wa misamaha

28 Misamaha kwa wasioweza kulipia gharama za matibabu, utatolewa na kulipiwa na Halmashauri baada ya kuzingatia utaratibu ufuatao:

(a) Serikali ya Mtaa au Kijiji katika vikao vyake itawatambua na kuwajadili na kupeleka kwa Kamati ya Afya ya Kata mapendekezo ya orodha ya majina ya watu wanaostahili kupewa msamaha kwa kutoa sababu zilizozingatiwa.

(b) Kamati ya Afya ya Kata itawajadili wale wasioweza kulipia gharama na kuthibitisha orodha yao na kuiwasilisha kwa Bodi kupitia kwenye Baraza la Maendeleo la Kata.

(c) Bodi ya Afya itapokea na kujadili mapendekezo husika na kuyawasilisha pamoja na gharama zake kwa Halmashauri kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi.

Adhabu

22 Mtu yeyote ambaye:

(a) atakwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi; au
(b) atafanya kitendo chochote ambacho kitazuia Bodi kufanya kazi zake kwa ufanisi; au
(c) atatumia vibaya mali na rasilimali za Mfuko na kusababisha kutofikia malengo ya Bodi; au
(d) atatumia vibaya madaraka aliyonayo kumzuia Afisa wa Bodi kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;
(e) atashindwa kwa uzembe kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia, atalipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kwenda jela kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na miwili au adhabu zote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Mhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, umebandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio la Kikao cha Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kilichofanyika tarehe 26 mwezi Juni, 2010.

Mhuri huo ulibandikwa mbele ya:

..............................

Bw. Jarvis A. Simbeye,
**MKURUGENZI WA MANISPAA**

..............................

Prof. Romanus C. Ishengoma,
**MSTAHIKI MEYA WA MANISPAA**

Nakubali,
Dodoma

Tarehe: 4/11/ ..........2010

..............................

Mhe. Mizengo P. Pinda (Mb),
**WAZIRI MKUU**